



Ukeketaji wa Wanawake/ Tohara

Ukeketaji wa Wanawake/ Tohara ni nini?

Ukeketaji wa Wanawake/ Tohara ni kukata au kubadilisha kimakusudi sehemu za siri za kike bila sababu yoyote ya kimatibabu. Una majina mengi, ikiwa ni pamoja na tohara, ukeketaji na upasuaji wa kitamaduni wa wanawake. Unadhuru afya ya wanawake na haufai.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Kwa ushauri na maelezo ya bila malipo na ya siri, piga simu kwa 1800RESPECT, nambari ya simu **1800 737 732**.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

Usaidizi wa kimatibabu unapatikana nchini Australia.

Ikiwa umeathiriwa na moja kati ya taratibu hizi unaweza kufikia huduma ya afya bila malipo na usaidizi nchini Australia. Madaktari, wauguzi, wataalamu wengine wa matibabu na walimu wanaweza kukusaidia.

Ikiwa unapanga kuwa na mtoto, unaweza kuongea na daktari, muuguzi au mtaalamu mwingine wa matibabu ili kupata usaidizi wa ziada ukiwa mjanzito na wakati una mtoto wako.

Ukeketaji wa Wanawake/ Tohara ni uhalifu mbaya nchini Australia.

Ukeketaji wa Wanawake/ Tohara ni kinyume cha sheria nchini Australia. Hii inajumuisha kumtuma mtu ng'ambo kufanyiwa upasuaji, au kuwezesha, kuunga mkono au kumhimiza mtu kufanyiwa upasuaji huu.

Mtu anayetokeleza uhalifu huu anaweza kufungwa jela, awe ni mwanamume au mwanamke.

Ikiwa umeathiriwa na moja kati ya mitindo hii, unahimizwa kutafuta msaada na hutaadhibiwa chini ya sheria ya Australia.

Kuna huduma na rasilimali zingine ambazo zinaweza kukusaidia.

Unaweza kupata maelezo kuhusu Ukeketaji wa Wanawake/ Tohara kwenye tovuti ya **National Education Toolkit for Female Genital Mutilation/Cutting Awareness** kwenye www.netfa.com.au.

1800RESPECT ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwa **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye www.1800RESPECT.org.au.

Ikiwa wewe, au mtu unayemjua, amepelekwa ng'ambo kwa ajili ya upasuaji huu au unafikiria yuko kwenye hatari ya kuondolewa nchini kwa ajili ya upasuaji huu, piga simu kwa 24/7 Consular Emergency Centre nambari ya simu **1300 555 135** (kutoka Australia) au **+61 2 6261 3304** (kutoka ng'ambo) au wasiliana na ubalozi wa ng'ambo wa Australia ulio karibu na wewe kwenye dfat.gov.au.

Je, unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.